# KISWAHILI PAPER 3

## EXPECTED QUESTIONS IN KCSE

**Comprises 6 KCSE prediction set exams (Class of KCSE March 2022).**

**For Marking Schemes Contact Mr Machuki 0795491185**

**Kenya Educators Contacts:**

**+254795491185**

**kenyaeducators@gmail.com**

**For More e-learning resources contact Kenya Educators via the contacts above.**

# PREDICTION 1

Jina_______________________________________Nambari ya Mtahiniwa: ________________

Shule: _____________________________________Sahihi: ______________________________

Tarehe: _____________________________

**102/3**

**KISWAHILI**
**Karatasi ya 3**

**FASIHI 102/3**

**KIDATO CHA NNE 2021**
**Muda: Saa 2 ½**

**Maagizo**

a) Andika jina lako, shule na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali manne pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la lazima.
e) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki ; yaani ; Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Fasihi Simulizi.
f) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya kiswahili.
g) Majibu yote sharti yaandikwe kwenye kijitabu cha majibu ulichopewa.
h) Karatasi hii ina kurasa nne zilizopigwa chapa.
i) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.
j) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja

Kwa matumizi ya mtahini pekee

| **Swali** | **Upeo** | **Alama** |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| 2 | 20 | |
| 3 | 20 | |
| 4 | 20 | |
| **Jumla** | **80** | |

**SWALI LA KWANZA, SWALI LA LAZIMA**

**SEHEMU YA A: USHAIRI- (Alama 20)**

Niokoa muokozi, uniondolee mashaka
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekitiri simanzi,ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka,nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka,nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka,nami nipate pumua
Naomba hisikitika,na mikono hiinua
Mtenda ndiwe moliwa,nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe moliwa,we ndiwe mola wa anga
Mazito kuyaondoa,pamoja na kuyatenga
Ukauepusha ukiwa,ya pingu zilonifunya
Nikundulia muwanga,nipate niyatakayo

Nikundulia muwanga,nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea,itoke kwangu moyoni
Mambo mema niegheshea,maovu nisitamani
Nitendea wa manani,nipate niyatakayo

Igeuze yangunia,dhaifu unipe mema
Nili katika dunia,kwa afia na uzima
Moliwa nitimizia,yatimize yawe mema
Nifurahike mtima,nipate niyatakayo.

**Maswali**

(a). Eleza bahari zozote mbili za shairi hili (alama 4)

(b). Eleza muundo wa shairi hili (Alama 4)

(c). Mshairi ametumia uhuru wake wa utunzi. Eleza mifano minne huku ukitoa mifano (alama 4)

(d). Andika ubeti wa pili katika lugha tutumbi (alama 4)

(e). Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili (alama.2)

(f). Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumika katika shairi (alama 2)

(i). Nimedhihika

(ii). Nifurahike mtima

**SEHEMU B: RIWAYA – ASSUMPTAMATEI - CHOZI LA HERI**

2. Haki za watoto hazitiliwi maanane katika jamii nyingi za kiafrika. Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea Riwaya ya chozi la heri (Alama 20)

**au**

3. "Kuukata mkono niliostahili kuubusu yalinifika ya kunifika" (Alama 20)

a. Eleza muktadha wa dondoo hili (Alama 4)

b. Eleza namna msemaji alivyoukata mkono aliostahili kuuibusu. (alama 6)

(alama 14)

c. Eleza tamathali ya usemi unaojitokeza katika dondoo hili. (alama.2)

d. Fafanua sifa nne za msemaji wa kauli hii (alama 8)

**SEHEMU C: TATHILIA KIGOGO NA PAULINE KEA**

4. ''Na hawa wafadhili wao nao lazima wavunje kambi zao. Sagamoyo twajiweza''

a. Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

b. Kwa kutolea mifano saba kwenye tamthilia eleza jinsi kauli hii ''Sagamoyo twajiweza'' ni kinaya ?

(alama 14)

c. Mbali na kinaya tambua mbinu nyingine ya kisanaa katika dondoo hili (alama 2)

**AU**

5. Jadili mbinu wanazotumia wanasagamoyo kujikomboa kutoka utawala dhalimu wa Majoka

(Alama 20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI - TUMBO LISILOSHIBA**

6. "… Ningeondoka…..mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana"

a) Eleza muktadha wa maneno haya (Alama 4)
b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili (Alama 2)
c) ''Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa

(Alama 9)

d). Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii (alama.5)

**AU**

7. (a). Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

(b). Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza,eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza

(alama 7)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8 (a) Miviga ni nini? (Alama 2)

(b) Fafanua sifa sita za miviga (Alama 6)

(c) Kwa nini jamii huthamini miviga (Alama 8)

(d). Onyesha udhaifu unaohusishwa na miviga (Alama 4)

# PREDICTION 2

**Jina**__________________________________________________________
**Nambari**_____________________________________________________
**Sahihi ya mtahiniwa**____________________________________________
**Tarehe**_________________________________________________________

**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3, FASIHI 1.**
**MUDA: 2 ½**
**<u>MAAGIZO</u>**

(a) **Jibu maswali manne pekee.**
(b) **Swali la kwanza ni lazima.**
(c) **Maswali hayo mengine matatu yachaguliww kutoka sehemu nne zilizobaki**
(d) **Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**

**SEHEMU A: Riwaya**

**1. LAZIMA**

**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**

"Hili lilimtia …………. uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke."

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)
(b) Taja suala linalodokezwa katika dondoo hili (alama 1)
(c) Kwa kutumia hoja <u>kumi na tano</u>, eleza namna suala ulilolitaja hapo juu 1 (b) linalijitokeza (ala. 15)

**SEHEMU B: Tamthilia**

**Kigogo (Pauline Kea)**

**Jibu swali la <u>pili</u> au la <u>tatu</u>**

2. "Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko……… huoni hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi?"

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b) Kufungwa kwa soko ni ukatili. Mbali na ukatili huu, toa mifano mingine ya ukatili kwenye tamthilia. (alama 9)
(c) Msemaji wa maneno haya ni mshauri mbaya. Thibitisha kutoka kwenye dondoo na kwingineko tamthiliani. (alama 7)

3. (a) Fafanua mbinu kumi anazotumia Majoka katika kuuendeleza uongozi wake(alama 10)
(b) Eleza namna mbinu ya <u>ishara</u> ilivyotumiwa katika tamthilia ya <u>Kigogo</u> (alama 10)

**SEHEMU C: Hadithi Fupi**

**Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine (Alifa Chokocho na Dumu Kayanda)**

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. "…………… Ningeondoka ….. mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana."

(a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

(b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili (alama 2)

(c) "Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa (alama 9)

(d) Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii (alama 5)

5. (a) Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza, eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza (alama 7)

**SEHEMU D: Fasihi Simulizi**

**6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! Kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasiotahiri,
Ama tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope
Wasichana wa kwetu na wa mbali

Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

Maswali;

(a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za kiuchumi za jamii ya wimbo huu (alama 4)
(b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? (alama 2)
(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha (alama 2)
(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume. Thibitisha kauli hii. (alama 2)
(e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii (alama 6)
(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii (alama 4)

**SEHEMU E: Ushairi (alama 20)**
**Jibu swali la 7 au la 8**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Kama dau baharini, duniya inavyoyumba,
Limeshamiri tufani, kila mmoja lakumba,
Viumbe tu hali gani!

Duniya yatishika, utahisi kama kwamba,
Vilima vyaporomoka, na kuvurugika myamba,
Viumbe tu hali gani!

Tufani hilo la kusi, languruma na *kutamba*,
Linapuliza kwa kasi, hapana kisichoyumba,
Viumbe tu hali gani!

Mujiwe ni kubwa sana, mfanowe kama nyumba,
Yazuka na kugongana, wala hatuna la *kwamba*,
Viumbe tu hali gani!

Mibuyu hata mivule, kama usufi na pamba,
Inarusha vilevile, *seuze hiyi migomba*
Viumbe tu hali gani!

Ni kipi kilotuliya, tuwazeni na kudumba,
Mandovu kiangaliya, yagongana na masimba,
Fisi wako hali gani!

Hata papa baharini, tufani limewakumba,
Walioko mikondoni, kila mmoja *asamba*,
Dagaa wa hali gani!

Mashehe wa mdaduwa, kwa ubani na uvumba,
Tufani hilo kwa kuwa, kusoze kwake kutamba,
Itokee afueni!
**(Shairi la 'Tufani' la Haji Gora Haji, katika *Tamthilia ya Maisha*, uk 62)**

**Maswali;**

(a) Taja na ueleze mikondo ya shairi hili (alama 4)
(b) Eleza dhamira ya shairi hili (alama 2)
(c) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
(d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)
(e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano. (alama 3)
(f) Onyesha matumizi ya idhini ya kishairi . (alama 3)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mjibu wa shairi hili (alama 2)
(i) Mdaduwa :
(ii) Kutamba :

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo Kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimtetea

Nao umande kumbusu miguuni;

Na miti yote hujipinda migogo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na  yeye kundelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha …….

Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho.
Kuna  jambo gani linalomridhisha?
Kama si kujua ni kutojua
Lait angalijua, laity angalijua!

**<u>Maswali:</u>**

a) Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. (alama 2)
b) Huku ukitoa mifano, onyesha aina <u>mbili</u> za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili (ala. 4)
c) Fafanua aina <u>tatu</u> za taswira ukirejelea ubeti wa pili (alama 3)
d) Maswali ya balagha katika shairi hili yanasisitiza maudhui yapi? (alama 2)
e) Kwa kutoa mifano, bainisha vipengele <u>vitatu</u> vya Kimtindo katika shairi hili (alama 3)
f) Eleza <u>toni</u> ya shairi hili (alama 2)
g) Bainisha nafsineni katika shairi hili (alama 1)
h) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)

# PREDICTION 3

**102/3**
**KISWHILI**
**KARATASI YA TATU**
**FASIHI**
**MUDA: 2 ½**

**JINA LA MTAHINIWA:………………………………………………………………………………**
**NAMBARI YA USAJILI:…………………  SAHIHI…………………………………………..**

**MAAGIZO**

i) *Jibu maswali manne pekee*

ii) *Swali la kwanza ni la lazima*

iii) *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki*

iv) *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja*

**1. FASIHI SIMULIZI: SWALI LA LAZIMA**

a) *Miviga ni nini?* Al.2

b) *Eleza sifa tano za miviga.* Al.5

c) *Fafanua hasara tatu za miviga.* Al.3

d) *Eleza changamoto tano ambazo mtafiti hukabiliana nazo anapokusanya data ya fasihi simulizi.* *Al.5*

-

e) *Eleza majukumu ya wimbo katika hadithi.* Al.5

**TAMTHLIA: KIGOGO**

**2. Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!**

***a) Eleza muktadha wa dondoo hili.*** ***Al.4***

***b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki.*** ***Al.4***

***c) Eleza matatizo yanayokumba safari inayorejelewa.*** ***Al.12***

3. **Tamthlia ya kigogo inazungumza kuhusu hali halisi katika mataifa mengi ya kiafrika. Jadili**. **Al.20**

4. **RIWAYA: CHOZI LA HERI**

"***Alikumbuka jinsi rafiki yake........alivyofishwa kwa njia hii. Akili yake ilimtambia kisa chenyewe kana kwamba inataka kumwonya (uk.120)***

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. Al.4

b) Bainisha tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. Al.4

c) Tathmini nafasi ya anayelengwa na kauli hii katika kuijenga riwaya hii. Al.12

5. a) Fafanua namna mbinu ya majazi ilivyotumiwa katika riwaya. Al.10
   b) Jadili maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii ukirejelea riwaya ya Chozi la Heri. Al.10

**6. <u>HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA</u>**

a) Eleza ufaafu wa anwani mapenzi ya kifuaurongo kwa kurejelea mhusika Penina. Al.10
b) Eleza nafasi ya elimu katika maisha ya wanajamii ukirejelea hadithi: Mtihani wa maisha. Al.10

7. a) **<u>Mame Bakari</u>**

*"**Una nini? Umeshtuka mwanangu! Unaogopa? Uaogopa nini?***

*a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. Al.4*

***b) Eleza sifa za mrejelewa. Al.6***

***c) Tambua mbinu mbili za lugha zilizotumika katika dondoo. Al.2***

***d) Eleza umuhimu wa msemaji.*** ***Al.4***

***e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki.*** ***Al.1***

***f) Fafanua maudhui katika swali la (e) kwa kurejelea hadithi nzima.*** ***Al.3***

**8. <u>USHAIRI</u>**
**<u>Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali</u>**

Alikwamba wako mama, kajifanya hupliiki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo!Hutaki
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo h adaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Manchangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mwenyewe!

**MASWALI**

***a) Eleza dhamira ya shairi hili.*** ***Al.2***

***b) Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kusisitiza ujumbe wake.Al.2***

***c) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi.***
***Al.4***

***d) Andika ubeti wa tatu katika lugha tutumbi.*** ***Al.4***

***e) Bainisha toni ya shairi hili.*** ***Al.2***

f) ***Kwa kutoa mfano mmoja mmoja, onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili.*** Al.4

***g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi.*** ***Al.2***

i) Mstahiki

ii) Hupuliki

# PREDICTION 4

**JINA……………………………………NAMBARI…………SAHIHI……..TAREHE…......**

**102/3**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**MUDA: SAA MBILI**

**MAAGIZO**

1) Jibu maswali manne pekee.
2) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
3) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki, yaani: tamthilia, fasihi simulizi, hadithi fupi na riwaya.
4) Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapa.
5) Kila mtahiniwa ni lazima ahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## SEHEMU YA A: SHAIRI -SWALI LA LAZIMA

**1.** M.S.Khatib:*Fungate ya Uhuru*

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata**

Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki

Lakini havishikiki

Ama havikamatiki

Ni kama jinga la moto

Bei juu

Maendeleo ya umma

Sio vitu gulioni

Kuviona madukani

Kuvishika mikononi

Na huku wavitamani

Kama tamaa ya fisi

Kuvipata ng'o

Maendeleo ya umma

Sio vitu shubakani

Dhiki ni kwa mafakiri

Nafuu kwa matajiri

Ni wao tu washitiri

Huo ni ustiimari

Lo! Warudia

Maendeleo ya umma

Ni vitu kumilikiwa

Na wanyonge kupatiwa

Kwa bei kuzingatiwa

Bila ya kudhulumiwa

Na hata kuhadaiwa

Hiyo ni haki

Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na supatu
Pasibakishwe na kitu
Huo usawa

Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la

Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiwa
Wazee hata vijana

**Maswali**

a) Huku ukitoa mifano, toa ithibati kuwa hili ni shairi huru (alama 5)
b) Mtunzi wa shairi hili alidhamiria nini? (alama 1)
c) Bainisha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili. (alama 2)
d) Andika ubeti wa nne kwa lugha ya kawaida (alama 4)
e) Eleza mambo yanayodhihirisha kuwa nchi imepiga hatua kiuchumi kwa mujibu wa shairi hili. (alama 4)
f) Eleza kwa kutoa mfano mbinu ambayo mtunzi wa shairi hili ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika ubeti wa sita. (alama 2)

g) Eleza aina ya urudiaji unaojitokeza katika ubeti wa pili na uonyeshe umuhimu wake katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU YA B: RIWAYA

**Assumpta K. Matei:** *chozi la Heri*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. Riwaya ya *Chozi la Heri* inasawiri adha zinayozikumba nchi za Kiafrika. Thibitisha kwa kutoa mifano mwafaka. (alama 20)

3. "Vijana hawapaswi kungojea kufanyiwa kila kitu. Tumewapa nyavu za kuvulia, nao wanaona wangoje kuletewa samaki!"

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua maudhui yanayodhihirika katika dondoo hili (alama 2)
   c) Tambua na ueleze mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili (alama 4)
   d) Eleza maafa yaliyomwandama msemaji wa kauli hizi (alama 4)
   e) Taja na ueleze sifa sita za msemewa (alama 6)

## SEHEMU YA C: TAMTHILIA

**P. Kea:** *Kigogo*

*Jibu swali la 4 au la 5*

4. Tamthilia ya *Kigogo* imesheheni mambo ya kukatisha tamaa. Thibitisha huku ukitoa mifano inayofaa. (alama 20)

5. "Walikuwa wanataka kukukanganya tu ili usiweze hata kuwakisia waliokudhuru"

   a) Eleza umuhimu wa msemaji katika dondoo hili (alama 4)
   b) Ni maudhui yapi yanayodhihirika katika dondoo hili? (alama 2)
   c) Msemewa na wenzake ambao wanapigania ukombozi pamoja walikumbana na vizingiti anuai. Eleza kwa kutoa mifano (alama 14)

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI

**A.Chokocho na D. Kayanda:** *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au la 7.*

***Ali A. Ali:*** *Ndoto ya Mashaka*

6. “Na kwa nini hazitaki kuukemea mfumo huu wa maisha? Mfumo wa mwenye nacho kuendelea kupata na msinacho kuendelea kukosa?”

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
   b) Fafanua maudhui mawili yanayodhihirika katika dondoo hili (alama 4)
   c) Tambua na ueleze sifa sita za msemaji (alama 6)
   d) Eleza athari ya “msinacho kuendelea kukosa” katika jamii husika (alama 6)

7. Fafanua jinsi suala la elimu limeshughulikiwa katika *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine* kwa kurejelea hadidhi zifuatazo:
   a) *Mapenzi ya Kifaurongo* (alama 5)
   b) *Shogake Dada ana Ndevu* (alama 5)
   c) *Mtihani wa Maisha* (alama 5)
   d) *Mwalimu Mstaafu* (alama 5)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Hapo zamani za kale paliishi mtoto katika kisima kimoja. Siku moja mtoto huyu aliokota kijiwe karibu na soko kuu. Kijiwe kilikuwa kikimeremeta kwa rangi mbalimbali na kilizingirwa na pete ya dhahabu.

Mtoto huyu na wenzake walianza kurushiana kijiwe hicho. Baada ya muda kilianza kuongezeka umbo na kuonekana kama kiwiliwili cha binadamu. Kikaanza kuwakimbiza wale watoto. Kutokana na ukelele wao, watu walikuja kutazama nini kilikuwa cha mno. Walipofika walikutana ana kwa ana na dubwana hilo. Lilizidi kuongezeka umbo na likawameza wote pamoja na mifugo wao. Wachache waliojaribu kukimbia liliwashika kwa mikono yake mipana na mirefu. Kwa bahati njema alikuwepo mama mmoja aliyeona hayo yote. Alikuwa mbali kiasi na hapo. Aliteremka kutoka kilele cha mlima na kuwapata wakulima makondeni na sawia akawajuza kuhusu kitendo kilichomwogofya sana. Wote wakaacha shughuli zao na wakatwaa silaha zao wakaelekea soko kuu.

Dude sasa lilikuwa limejilaza baada ya shibe, wakulima wale walichagua watu sita ambao walijulikana kwa ushujaa wao. Pamoja walilinyemelea lile nyangarika na kulikata mara moja. Lilitoa mkoromo mkuu kabla halijakata kamba. Punde, wanakijiji kwa uangalifu mkubwa walitoboa tumbo lake wakitarajia kupata maiti za wapenzi wao pamoja na mifugo wao. Wote walijawa na furaha kuu walipoona wapenzi wao wakijichomoza kutoka tumboni, mmoja baada ya mwingine hadi akatoka yule wa mwisho. Mbuzi, kondoo na ng’ombe wote walitoka mmoja mmoja.

Siku hiyo kuliandaliwa sherehe ya kumshukuru Muumba kwa wema wake. Watoto walishauriwa wasithubutu kuchezea vitu wasivyovijua.

**Maswali**

a) Ainisha kipera hiki cha hadithi (alama 1)

b) Fafanua mambo manne yanayodhihirisha kuwa kipera hiki ni sanaa. (alama 4)

c) Mwasilishaji bora wa kipera hiki anafaa kuwa na sifa gani? Eleza zozote nne. (alama 4)

d) Onyesha mifano miwili ya fantasia katika hadithi hii. (alama 2)

e) Eleza majukumu manne ya tungo hizi kwa wanajamii (alama 4)

f) Eleza majukumu matano ya mtindo uliotumiwa kuanzisha hadithi hii. (alama 5)

# PREDICTION 5

**JINA..........................................................................NAMBARI.................................................**

**SHULE.................................................................... SAHIHI.............................. TAREHE.................**

**102/3 (FASIHI)**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2½**

***Hati ya kuhitimu kisomo cha sekondari Kenya (K.C.S.E)***

**102/3(FASIHI)**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA 3**

**MUDA: SAA 2**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA**

**a.Jibu maswali <u>manne</u> pekee**

**b. Swali la kwanza ni la lazima**

**c. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani: Tamthilia, Hadithi fupi, ushairi na fasihi simulizi.**

**d. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**

**Kwa matumizi ya mtahini pekee.**

| Swali | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

**SEHEMU YA A: RIWAYA YA : CHOZI LA KHERI(ASSUMPTA .K. Matei)**

**1.Swali la Lazima**

A. ``Kumbe hata wewe shemeji..............upo?''
``ndio tu hapa na wengi''
i.Eleza muktadha wa dondoo hili. alama 4
ii.`Wengi ' wanaorejelewa katika dondoo hili walikumbwa na matatizo yapi? alama 8

B.``Kule kulazimika kupapasa kwenye giza kutafuta............''
Mrejelewa katika kauli hii anayafichua maovu yapi katika jamii? alama 8

**SEHEMU YA B. TAMTHILIA KIGOGO ( Pauline kea)**

2.``Huu moyo wangu wa huruma nao..............................''
i.Eleza muktadha wa dondoo hili. alama4
ii.Fafanua sifa za msemaji. alama 4
iii.Onyesha kinyume kinachojitokeza katika dondoo hili. alama 12

3.Vijana katika tamthilia ya kigogo wamesawiriwa kwa jicho hasi. Fafanua alama 20

**SEHEMU YA C. HADITHI FUPI**
**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE ( WAHARIRI: A CHOKOCHO NA D. KAYANDA)**

4. `..........Lakini shogake................. shogake.................. shogake dada nikamwona ana ndevu'.

a. Eleza muktadha wa dondoo hili. alama 4
b. Bainisha sifa tatu za `shoga ' anayezungumziwa katika dondoo hili. alama 6
c.Jadili umuhimu wa `dada' anayerejelewa katika kuendeleza dhamira ya hadithi. alama 10

5.``Wahusika katika hadithi shibe inatumaliza wanatumia uhuru wao vibaya.''Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano. alama 20

**SEHEMU YA D. USHAIRI**

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

1. Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na ng`ambo,

Kwaani ngoja `mesikia, inaumiza matumbo,
Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimombo,
Yafaa jihadharia, maisha yas`ende kombo.

2. Maisha yas`ende kombo, kututoa yetu ari,
Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari.

3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahama,
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatuuma
Watoto tunayo mori, ni lini mtajakoma?

4. Ni lini mtajakoma, na pombe siso halali?
Sio baba sio mama, mbona ny`hamtajali?
Mwafaja nzi twasema, mwatuacha bila hali
Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila saa mwapigana
Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona
Mwatusumbua akili, twaumia ten asana
Acheni na ukatili, kwani upendo hamna.

6. Kwani upendo hamna, kama mbwa mwatuchapa
Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa
Pa kujificha hatuna, tumebaki tukitapa

7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,
Mwatubaka na kuapa, kutung`ata nyi' majitu,
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukufu

8. Mtakoma utukufu, na kutumia mikiki
Na tabia zenye kutu, tumechoka nayo chuki
Hatutakubali katu, kutendewa yenye siki
Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki.

a. Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. alama 2

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

b. Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. alama 4

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

c. Taja nafsineni katika shairi hili. alama 1

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

d. Eleza bahari nne zinazowakilishwa katika shairi hili alama 4

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

e. Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari. alama 4

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

f. Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. alama 3

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

g. Huku ukitoa mfano, taja mfano wa uhuru wa mshairi ambao ume tumiwa katika shairi hili. alama 2

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

..........................................................................................................................................................

7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Mlipozinduka,
Mkaungana na kushikana

Kwa nguvu moja mkavuta, mkavuta
Mdogo akivuta na mkubwa anavuta, nyote mlipovuta
Si makubwa mlitenda!
Babu yangu kajiunga
Babu yako akaja Mmoja alipokohoa, mwenzake akampokea
Homa hiyo kaenea ja moto wa kiangazi
Mau mau wakazalika, nywele ndefu zilizosokotana
Si mkoloni aliondoka!

Ubinafsi upigiwa teke
Kimoja wakajiona
Wala
Si viungo tofauti vya mwili mmoja
Si taifa lilisimama!
Doa ikaitwa Dola
Na wimbo wa taifa, kitambulisho
Vazi la taifa kashonwa
Bendera ilipepea!

Mbona msambaratiko?
Sasa
Mbona wa kwenu tu?
Vicheko si vicheko, bashasha juu ya bashasha
Wa ndani busu moto moto
Wengine soma mgongo!
Na kuta wajijengea, za mawe na za miba
Taba samuyo hela ngapi, waso wakalipe?

Na ndimi zatema ndimi
Miale ya kuunguza!
Wakweapo ulingoni
Wagongesha huyu na yule
Viongozi maluuni, waajiri kikabila
Kiongozi maluuni, cheo wakweza kwa kabila
Maluuni maluuni
Adhabu zako za kikabila!
Twajenga ukibomoa, mzalendo sampuli gani?

Nyoyo zetu lako shamba
Wazichimbua hisia, na mashimo wapanda chuki
Fitina ndo maji yako, Wanyunyiza na kwa bidii
Tofauti za kikabila, na lawama mzomzo
Pindi uwakapo moto, huyoo watakomea!
Kiongozi maluuni.

a. Huku ukitoa mifano mwafaka,eleza sifa za shairi huru zinazojitokea katika shairi hili. alama 6

..........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

b. Fafanua aina tatu zamsambaratiko unaozungumziwa katika shairi hili. alama 6

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

c. Bainisha mbinu sita za kifasihi zinazojitokeza katika shairi hili. alama 6

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

........................................................................................................................................................

d. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi hili alama 2
i.Bashasha
ii.sampuli

**SEHEMU YA E. FASIHI SIMULIZI.**

Katika jamii ya Itaso watoto pacha huchukuliwa kama mkosi. Kwa hivyo, hubidi sherehe maalum ifanywe ili kutakasa wazazi wa watoto hawa. Sherehe hii hufanyika siku tatu baada ya kuzaliwa kwa watoto mapacha.

a. Tambua kipera kinachodokezwa na maelezo haya na ukifafanua. alama 2

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

b. Fafanua umuhimu wa kipera cha fasihi ulichotambua katika (a) alama 8

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

..............................................................................................................................................

c. Fafanua sifa zozote tano za soga. alama 5

..............................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

d. Ni changamoto zipi zinaweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa soga nyanjani. alama 5

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

....................................................................................................................................................

# PREDICTION 6

**102/3**
**KISWAHILI FASIHI**
**KARATASI YA TATU**
**MUDA: SAA 2 ½**

***Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)***

**102/3**
**Fasihi ya Kiswahili**
**Karatasiya 3**
**MUDA: SAA 2 ½**

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

1) Andika jina lako, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.
2) Karatasi hii ina sehemu tano: A, B, C, D na E.
3) Jibu maswali ***manne pekee***. Kila swali lina alama ishirini.
4) Swali la ***kwanza*** ni la ***lazima***.
5) Chagua maswali mengine ***yoyote matatu*** kutoka sehemu zilizosalia; B, C, D ama E.
6) Usijibu maswali ***mawili*** kutoka ***sehemu moja***.
7) Majibu yote yaandikwe kwa ***Kiswahili*** katika ***karatasi ya majibu*** uliyopewa.

***Sehemu hii imehifadhiwa kwa matumizi ya mtahini pekee***

| **SWALI** | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **UPEO** | **20** | **20** | **20** | **20** | **20** | **20** | **20** | **20** |
| **ALAMA** | | | | | | | | |

**JUMLA**

| | |
|---|---|
| **UPEO** | **80** |
| **ALAMA ZA MTAHINIWA** | |

***Karatasi hii ina kurasa 6 zilizopigwa chapa.***
***Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa.***
***na kuwa maswali yote yamo.***

## SEHEMU YA A

**TAMTHILIA: KIGOGO**

(Pauline Kea)

1. "Ni laghai siwaamini. Wanasema wanakwenda huku na mara…"
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Alama 4)
   b) Eleza mbinu ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (Alama 2)
   c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji. (Alama 6)
   d) Fafanua jinsi wanaorejelewa na mzungumzaji walivyo laghai. (Alama 10)

## SEHEMU YA B

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

(Assumpta K. Matei)

Jibu swali la ***Pili*** au la ***Tatu***

2. "Watu husema kuwa binadamu hawawi sawa ila kifoni…"

   a) Eleza muktadha  wa maneno haya. (alalama 4)

   b) Tambua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)

   c) Eleza sifa na umuhimu wa mzungumzaji wa maneno haya. (alama 6)

   d) Thibitisha kuwa hakuna usawa baina ya wanadamu. (alama 8)

*Au*

3. Jadili nafasi ya sehemu zifuatazo katika riwaya ya Chozi la Hari:
   (a) Hotuba (alama 10)
   (b) Uozo katika jamii  (alama 10)

## SEHEMU YA C

**HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

(Alifa Chokocho na Dumu Kayanda- Wahariri)

Jibu swali la ***Nne*** ama la ***Tano***

**NDOTO YA MASHAKA**

4. "Sasa nimechoka mja. Nimechoka hata naradua kufa kuliko kuishi."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Taja mbinu mbili za lugha katika dondoo hili. (alama 4)
   (c) Mzungumzaji alikuwa na haki ya kuradua kufa. Thibitisha. (alama 12)

*Au*

5. Ukirejelea hadithi zozote nne katika diwani ya Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine, eleza jinsi maudhui ya Mapenzi na ndoa yanavyojitokeza (alama 20)

**SEHEMU YA D**
**USHAIRI**

***Jibu swali la sita ama la saba***

***6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali***

Naogopa, kukupa wangu mtima, sitaki mie nilie
Naogopa, kutoa yangu kalima, eti wewe utulie
Naogopa, ninashindwa kusimama, wewe pete unitie
Naogopa, wanaume wanauma, ja panya wapulizie.

Naogopa, kwita wako mama mama, nami anikaripie
Naogopa, sipendi nyingi dhuluma, za wanaume nilie
Naogopa, kushinda nimeinama, goti mume nipigie
Naogopa, za mkemwenza hujuma, matusi anipatie.

Naogopa, uchungu ukiniuma, mwana nikakuzalie
Naogopa, kupigwa kama ngoma, ndiposa nikatulie
Naogopa, kila kitu kunisoma, ndo hela unipatie
Naogopa, kuitwa mwizi wa sima, ila nikuandalie.

Naogopa, dadazo kuwaandama, udaku wakanitie
Naogopa, kuuleta uhasama, mimi mnipiganie
Naogopa, koritini kusimama, mali tukashindanie
Naogopa, kumwaga wenu mtama, kuku niwamiminie,

Naogopa, naogopa ninasema, yabidi uvumilie
Naogopa, nawe babu kusimama, eti ndoa niingie
Naogopa, ndoto zangu kuzizima, hili doa nijitie
Naogopa, <u>taa yangu kuizima</u>, mwingine jitafutie.

*(Meja S. Bukachi- Uketo wa Ushairi uk 24)*

**MASWALI**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (Alama 1)
b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (Alama 1)
c) Nani nafsi nenewa katika shairi hili? (Alama 1)
d) Taja tamathali za lugha zilizotumika katika shairi hili. (Alama 2)
e) Fafanua uhuru wa ushairi alioutumia malenga. (Alama 2)
f) Weka shairi hili katika bahari mbalimbali. (Alama 3)
g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (Alama 4)
h) Kwa nini nafsi neni anasita kuchukua hatua? (alama 4)
i) Vifungu vifuatavyo vina maana gani katika shairi? (alama 2)
   i. Taa yangu kuizima
   ii. Dhuluma

***Au***

***7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tulichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisha kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,
Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu,
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,

Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa,
Iwapo wewe ni mume,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri

**Maswali**

(a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha. (alama 2)

(b) Ni nani anayeimba shairi hili na analiimba kwa nani ? (alama 2)

(c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi ya kiume (alama 2)

(d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (alama 4)

(e) Taja shughuli zozote **mbili** za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (alama 2)

(f) Eleza kwa mifano, uhuru wa kishairi katika shairi hili (alama 4)

(g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (alama 4)

(i) Mbari
(ii) Msununu

(iii) Ngariba
(iv) Uvundo

## SEHEMU YA E

## FASIHI SIMULIZI

***Soma utungo ufatao kisha ujibu maswali***

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,
Nami ndiye niliompa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu na waone chozi langu, wasikie kilio changu,
Mizimu na waone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!
***(Kutoka: Assumpta K. Matei- Fani ya Fasihi Simulizi, uk 145)***

**Maswali**

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 2)
(b) Jinsia ya nafsi neni ni gani? (alama 2)
(c) Eleza sifa zozote sita za kipera hiki cha fasihi simulizi. (alama 6)
(d) Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii. (alama 4)
(e) Fafanua njia sita jinsi jamii ya kisasa inavyojaribu kuendeleza fasihi simulizi. (alama 6)